



United Nations  
Educational, Scientific and  
Cultural Organization

Organisation  
des Nations Unies  
pour l'éducation,  
la science et la culture

Organización  
de las Naciones Unidas  
para la Educación,  
la Ciencia y la Cultura

Организация  
Объединенных Наций по  
вопросам образования,  
науки и культуры

منظمة الأمم المتحدة  
للتربية والعلم والثقافة

联合国教育、  
科学及文化组织

## Ujumbe kutoka kwa Bi Irina Bokova, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO, Siku ya Urithi wa Afrika Duniani, Mei 5, 2017

Siku ya Urithi wa Afrika Duniani ni fursa ya kusherehekea utajiri wa utamaduni na asili ya bara, asili ya ubinadamu. Pia ni wakati unaofaa kutoa onyo kwa ajili ya ulinzi wa urithi wetu. Leo maeneo ishirini na tatu (23) ya Afrika yapo kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia ulio katika Hatari – Mji Mkongwe wa Ghadamès, Hifadhi ya Kahuzi-Biega, na Hifadhi ya Asili ya Mlima Nimba Mkali – ziko hatarini kutoweka kama hatutachukua hatua za haraka ya kuzilinda. Kila mmoja ana jukumu hilo.

Hatua ya kulinda urithi barani Afrika sasa, inaunda maisha yetu ya baadaye. Kusaidia jamii - na hasa vijana - ili kukuza na kuendeleza rasilimali nyingi za kitamaduni na asili ina maana ya kuandaa mipango ya muda mrefu, inayozinagatia maendeleo itakayoletwa na umoja na ushikamano wa jamii. Maeneo ya Afrika yanalindwa zaidi na jamii zinazoishi kando yao kila siku na kupata utambulisho wao kupitia huu urithi na kuendesha maisha yao kutokana na mapato wanayopata kupitia kwao. Usimamizi wao ni endelevu zaidi ukiongozwa na vijana ambao wanatambua umuhimu wao. Azimio la Ngorongoro, lililopitishwa mwaka 2016, linahamasisha kuendeleza jukumu la jamii, hasa ya vijana wanaume na wanawake, katika usimamizi wa maeneo ya urithi wa dunia. Ujumbe huu unaendelea kuwa muhimu leo.

Ulinzi imara unahitaji elimu, habari sahihi na utafiti. Hii ndiyo sababu UNESCO katika kutekeleza wajibu wa kulinda urithi wa Afrika inasimamia katika kazi yake ya kuelimisha na kusambaza uelewa wa umuhimu wa urithi kuptia elimu ya maadili ya kuvumiliana, kuheshimiana na uelewa wa tamaduni. Katika Afrika, UNESCO inafanya kazi ya kuimarisha usimamizi wa maeneo katika programu ya chuo kikuu na mafunzo.

Leo, ninawaomba wadau wote wa Afrika, nchi zote, vyama vya kiraia na vya kijamii kuchukua jukumu la ulinzi wa mali ya Bara la Afrika zisizolinganishwa na bara jingine kwa utajiri. Ningependa kuwashukuru kwa dhati, wale wote wanaopambana kila siku, wakati mwingine hata kuhatarisha maisha yao, ili kulinda na kushiriki urithi huu wa kipekee wa binadamu wote. Hii inaashiria nyayo zetu za zamani kuwakilisha msingi imara wa maadili, vigezo na kujiamini kwa maisha ya baadaye. Afrika ni tajiri kwa haya, na maendeleo chanya yenye tija kwa Afrika yanategemea kuendeleza urithi wa bara la Afrika.

UNESCO  
7, Place de Fontenoy  
75007 Paris  
France

Website:  
[www.unesco.org/new/en/  
unesco/about-us/who-we-  
are/director-general/](http://www.unesco.org/new/en/unesco/about-us/who-we-are/director-general/)